

## Utata katika Uainishaji wa Fasihi Simulizi: Hali ya Sasa na Mustakabali Wake

*Fred Wanjala Simiyu*  
*Chuo Kikuu cha Kibabii, Kenya*

### Ikisiri

Makala haya yanajadili suala la vigezo vinavyotumiwa kuainisha fasihi simulizi katika lugha tofautitofauti. Utafiti wetu ulichochea na masuala kadha: Je, baadhi ya maumbo yaliyozoeleka kuitwa tanzu au vipera vya Fasihi Simulizi ni sehemu ya Fasihi? Yaani, mafumbo, michezo jukwaani, mawaidha, maigizo, mazungumzo na mivigha ni tanzu au vipera vya Fasihi Simulizi kweli? Je, katika lugha nyinginezo, ‘tanzu’ au ‘vipera’ hivi vipo na vinaitwaje? Je, fasihi ni nini? Katika kujibu maswali haya na mengine, makala haya yanabainisha kwamba, masuala haya sita sio vipera wala tanzu za Fasihi Simulizi bali, mengine ni majukumu ya Fasihi Simulizi; mbinu zinazotumiwa kuwasilisha Fasihi Simulizi; na majukwaa yanayoruhusu utendaji wa Fasihi Simulizi. Kwa kuongozwa na Nadharia ya Tanzu, mfano mzuri ni ‘utanzu’ unaoitwa ‘mivigha’ haupo; badala yake ‘utanzu’ huu unafaa kuangaliwa kama jukwaa linaloruhusu utolewaji wa tanzu mbalimbali zinazolingiliana katika utendaji. Hii ni kwa sababu, mivigha ni sawa na basi linalobeba tanzu na vipera kama abiria kuelekea sehemu mbalimbali. Hii ina maana kuwa, ‘mivigha’ sio utanzu wala kipera bali ni kongoo la Fasihi Simulizi linaloelea na ambalo ‘tanzu’ mbalimbali hupanda jukwaani na kutekeleza wajibu wake, na baadaye kushuka au kushushwa ili kupisha tanzu zingine; nazo zitekeleze wajibu wake. Upandaji na ushukaji huu wa tanzu hizi huiwezesha mivigha husika kutekeleza wajibu wake wa ujumla.

Istilahi Muhimu: Tanzu, Vipera, Mafumbo, Maigizo, Mazungumzo na Mivigha.

### Utangulizi

Fasihi Simulizi ni somo linalofundishwa katika ngazi mbalimbali za elimu hapa Afrika Mashariki. Ili somo liweze kueleweka vizuri, ni vyema lifundishwe kwa mpangilio na kwa hatua madhubuti. Fasihi Simulizi ya Mwafrika ni hazina kuu ya maarifa iliyojengeka kwa miaka na mikaka. Uainishaji wa Fasihi Simulizi ya

Kiafrika umefanywa kupitia utafiti wa wageni na wenyeji wanaongozwa na mikabala ya kigeni. Tunalenga kutathmini upya muainisho wa Fasihi Simulizi wa kimabavu na wa kigeni uliozoeleka. Watafiti hawa wametoa mchango mkubwa katika kupanua mawanda ya Fasihi Simulizi kama hazina kuu ya maarifa inayoendelea kukua kila uchao. Hata hivyo, mchango wao umeathiriwa zaidi na maarifa waliyoyapata shuleni. Masomo yao yanawafanya waiangalie Fasihi Simulizi kama mfumo unaoweza kuainishwa na kuchanganuliwa katika tanzu zinazojitegemea na kujikamilisha kiutendakazi bila kuingiliana na tanzu zingine. Utafiti huu umebainisha kuwa, ni vigumu kuweka mipaka dhahiri kati ya tanzu za Fasihi Simulizi ya Kiafrika kwa sababu, kila utanzu una sifa tofautitofauti za kiutanzu zinazouwezesha uwekwe katika vikundi zaidi ya kimoja wakati wa uainishaji. Baadhi ya wataalam walioshughulikia taaluma ya Fasihi Simulizi pamoja na Senkoro (2011), Simiyu (2011), King'ei (2005), Wamitila (2003), Kimani na Chimera (2002), Mulokozi (1996), Okpewho (1992), Madumulla (1995), Kirumbi (1975) na Finnegan (1970).

### **Nadharia ya Tanzu**

Makala haya yameongozwa na Nadharia ya Tanzu. Nadharia ya Tanzu iliasisiwa na Wayunani walioamini kuwa, aina ya ushairi ilitokana na aina ya malenga wa shairi husika. Aristotle alidai kuwa, kuna aina mbili kuu za mashairi kwa mujibu wa aina ya malenga: mashairi haswa yanayosawiri hali halisi ya watu mashuhuri katika tabaka la juu na hutungwa na malenga mashuhuri. Aina ya pili ni mashairi uchwara yanayotungwa na malenga ovyo na yanasakidi hali duni ya walalahoi walioko katika tabaka la chini na ambayo hutumia sana mbinu ya tashtiti. Muainisho huu una upungufu kwani unatumia kigezo finyu chenye ubaguzi. Derrida (1980) katika makala yake “The Law of Genre” anasema sifa zinazoutambulisha utanzu fulani zinaweza pia kutumika katika kupinga muainisho unaoutambua utanzu wenyewe. Aidha, Cohen (1986) katika makala yake “History of Genre” anasema utanzu huibuka, hubadilika na hata kutoweka kwa sababu za kihistoria. Kwa hivyo, uumbaji wa utanzu ni mchakato wazi na wala sio fungu (kwa maana ya aina zenye mipaka bainifu).

Kila kijenzi huathiri utanzu husika ndani ya mchakato wa ubunaji wake kwa kuongeza, kuondoa au kubadili viambato. Haya yote yanatokea kwa sababu mbili kuu: utenganishwaji na utangamano wa vijenzi ndani ya utanzu mmoja. Maoni haya kuhusu uainishaji wa tanzu yalikusanywa na kutumiwa katika kuzalisha Nadharia ya Tanzu na akina Ben-Amos (1976) na Berkenkotter na Huchin (1995). Kwa ujumla, wao wanadai kuwa, fasihi inaweza kuainishwa kwa kuzingatia vigezo vinne: maudhui, ujitoshelezaji, utendakazi na sifa bia. Kwa ujumla basi, baada ya kutazama maoni ya wataalam mbalimbali waliokuwa na mitazamo tofauti kuhusiana na Nadharia ya Tanzu, mihimili ifuatayo imebainika:

Kwanza, tanzu ni zao la desturi za jamii kwani tanzu ni mali ya jamii. Tanzu zinatazamwa kama zao la desturi na imani za jamii husika. Swale (1990) anasema kuwa utanzu unasaidia waanajamii kufanikisha nia au lengo lao. Muller (1991) anasisitiza umuhimu wa nia na jamii katika Nadharia ya Tanzu hivyo kutoa fasili ya tanzu kama matendo ya kijamii. Tanzu kwa hivyo ni dhana ya kiuneni wala sio ya kiisimu. Pili, tanzu hudumu katika mabadiliko. Yaani tanzu za Fasihi Simulizi lazima zibadilike kwa sababu washiriki, vifaa, muktadha na siasa za vikundi vya kijamii hubadilika na hivyo kuathiri tanzu katika jamii husika. Hii hali ya kubadilika kwa utanzu umesababisha Scheyer (1994) kufaili tanzu kama kitu kilicho kinyumbufu. Tatu, uhusiano kati ya tanzu na vikundi vya jamii hujengana na kuelekezana. Maarifa ya desturi za jamii huelekeza watoaji wa kazi za kifasihi katika kazi zao. Hii ina maana uelewa na ukubalikaji wa tanzu unatokana na tajiriba ya pamoja ya jamii husika. Nne, tanzu sio visiwa vilivyojitenga. Vikundi vya jamii hutumia mkusanyiko wa tanzu kutimiza malengo au nia zao. Utanzu katika mkusanyiko huu huingiliana kwa njia kadhaa kama vile kujibu utanzu mwingine au kuukamilisha. Uhusiano huu unadhibitisha mihimili ya mwingianotanzu katika tanzu mbalimbali. Kwa hivyo, mchambuzi wa Fasihi Simulizi anastahili kuangalia mkusanyiko wa tanzu wala sio utanzu moja moja. Tano, Nadharia ya Tanzu ni dhana ya utambulisho, kuweka kazi za kifasihi katika kategoria ya vikundi mbalimbali, hivyo lengo kuu la nadharia hii ni uainishaji. Maana yake ni kwamba, uundaji wa tanzu huambatana na uundaji wa kanuni na sheria zinazotambulisha tanzu zenyewe. Sita, tanzu za Fasihi Simulizi hazina mipaka dhahiri ya kuzitanganisha. Mipaka hiyo dhahania huvujwa kupitia kwa mwingilianotanzu, ambao ni hali anayoruhusu tanzu mbalimbali za Fasihi Simulizi kuvunja mipaka ya kiutanzu na kuchanganyikana wakati wa utendaji.

### **Uainishaji wa Fasihi Simulizi**

Fasihi Simulizi inaweza kuainishwa kwa kutumia vigezo mbalimbali, kama ilivyofafanuliwa na Nadharia ya Tanzu. Vigezo hivi ni pamoja na namna ya uwasilishaji, muundo, walengwa, maudhui na wahusika. Wataalam wengi wa kigeni na wenyeji wametumia nadharia na mbinu za Ki-Aristotle katika uainishaji wao wa Fasihi Simulizi ya Kiafrika. Wataalam hawa ni pamoja na Finnegan (2012), Ong' (1982), Bayo na Abadul Rashid (2012), Liz na Graham (1995), Okpwho (1992), Namulundah (2012) na wengine. Aidha, Waswahili wana fasihi yao ambayo imeainishwa na wataalam mbalimbali: Kirumbi (1975), Mulokozi (1996), Wamitila (2003), Ngure (2003) na King'ei na Kisovi (2005) na Simiyu (2011). Uainishaji wa wataalam hawa unadhihirisha utata wa aina mbalimbali.

### **Utata wa Kiistilahi**

Wataalam tuliwapitia wametofautiana sana katika uainishaji wa tanzu na vipera vya Fasihi Simulizi. Utofauti huu wa uainishaji unawaacha wanafunzi na walimu

wa Fasihi Simulizi katika njia panda wasijue wa kumfuata. Tofauti hizi huanzia kwenye matumizi ya istilahi tofauti zinazoeleza kitu kilekile! Swali ni je tutumie istilahi gani kwa maana gani katika muainisho wa Fasihi Simulizi? Ni tanzu, vipera, kumbo, aina, makundi, fani, michepuo au nui? Istilahi hizi zimetumiwa na wataalam tofauti kwa maana ama tofauti au moja, mathalan: Kirumbi (1975:12) anasema:

Fani ni utanzu kwa hivyo tunapotaja fani za Fasihi Simulizi tumekusudia tanzu za Fasihi Simulizi.

Naye Ngure (2003:10) anadai:

Fasihi Simulizi imegawanyika katika vipera vitatu vikuu na kila kipera kina vijipera vidogo vidogo.

Isitische, Mulokozi (1996:11) anasema:

Tunaweza kuzigawa tanzu za Fasihi Simulizi katika makundi makuu sita. Tuliweza kuona kuwa Fasihi Simulizi huweza kuwekwa katika kumbo au michepuo sita. Baadhi ya kumbo huweza kuwa na nui na kila nui huwa na tanzu kadha.

Kadhalika, Wamitila (2003:1) anasema:

Kuna makundi kadha ya Fasihi Simulizi. Kila kundi lina vijitawi au vipera kadha.

Kwa mujibu wa maelezo ya wataalam hawa, ni dhahiri kwamba huenda wanatumia istilahi tofauti kusema kitu kilekile au wanatumia istilahi zinazofanana kusema vitu tofauti. Inatubidi tuchunguze maana ya istilahi hizi: Longhorn (2011) wanasema:

- Tanzu – tawi la mti au shirika au kiwangi.
- Nui – aina tofauti za vita au namna.
- Kumbo – tendo la kuchukua vitu au watu wengi pamoja.
- Mchepuo – fani ya taaluma mahsusi au ifundishwayo shuleni.

Aidha, Wamitila (2003) anasema:

- Utanzu – hutumiwa kuelezea au kurejea aina ya kazi mbalimbali za kifasihi.
- Fani – muundo au mpangilio wa kazi fulani ya kifasihi au hata sehemu zake.

Naye Senkoro (2011) anadai:

Fani ni ule ufundi wa kisanaa anaotumia msanii katika kazi yake.

Baada ya kuangalia maana ya istilahi hizi ambazo zimetumiwa na wataalam mbalimbali wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili, ni wazi kwamba wasomaji wao wanaweza wakachanganyikiwa. Istilahi hizi zimetumika bila kutolewa ufafanuzi

na wakati mwingine zinatumiwa kama visawe vinavyotofautiana. Kwa mfano, Kirumbi (k.h.j) anatumia maneno *fani* na *utanzu* kama visawe kimakosa. Utafiti wetu unapendekeza matumizi ya *tanzu* kwa maana ya matawi makuu ya Fasihi Simulizi na *vipera* kwa maana ya vijitawi chini ya kila utanzu. Kwa maoni yetu, neno ‘fani’ haliwezi kutumiwa kwa maana ya matawi ya Fasihi Simulizi kwani lina maana yake maalum katika uwanja wa fasihi. Kadhalika, maneno nui, mchepuo na kumbo yatumiwa katika tasnia nyinginezo. Matumizi ya istilahi moja kwa maana moja itawasaidia wanafunzi na walimu wa Fasihi Simulizi kuweza kusawazisha usomaji wao.

### Utata wa Kimipaka

Mulokozi (1996) anakiri kabisa kuwa ameanisha Fasihi Simulizi ya Waswahili katika tanzu au kumbo sita mahsusi kwa ajili ya kufundisha: semi, mazungumzo, masimulizi, maigizo, ushairi simulizi na ngomezi. Muainisho huu unaeleweka kwa urahisi kwa wasomaji kwani ni wa moja kwa moja. Hata hivyo, kuna mkanganyiko katika uainishaji wa Mulokozi; ametenga ngomezi kama kumbo linalojisimamia, lakini katika maelezo yake, ngomezi inabainishwa katika utanzu wa ushairi simulizi. Ikiwa hivyo, basi kumbo zake hazipaswi kuwa sita badala yake ni tano. Mulokozi pia ameanisha nyimbo katika nui nne kuu: tumbuizo, tukuzo, chapuzo na tenzi au tendi. Anasema kuwa, tumbuizo ni nyimbo za kuliwaza au kufurahisha watu kwenye matukio mbalimbali. Ametoa nyiso kama mfano wa tumbuizo. Hapa kuna tatizo, maana si nyiso zote hulenga kuliwaza na kufurahisha. Kwa mujibu wa maelezo yake, tukuzo ni nyimbo zinazotukuza au kudhihirisha utukufu na ufahari wa jambo fulani. Kuna nyiso ambazo hutukuza mila, watu au matukio mbalimbali katika jamii. Basi, nyiso kama hizi zinapaswa kubainishwa kama aina ya tukuzo.

Halikadhalika, Wamitila (k.h.j) ameanisha fasihi simulizi ya Waswahili katika tanzu nne: simulizi au hadithi, maigizo, ushairi na semi pamoja na kuwepo kwa vipera mbalimbali kwa kila utanzu. Sasa, kipera cha ngonjera kinajitokeza katika tanzu mbili tofauti (ushairi na maigizo) bila maelezo yoyote. Naye Ngure (2003), anasema kuwa, ameanisha Fasihi Simulizi ya Waswahili ili kurahisisha maelezo katika kitabu chake. Ameanisha Fasihi Simulizi katika vipera vitatu vikuu: utambaji au usimulizi, tanzu fupi na ushairi simulizi. Kwa kweli, uainishaji wake ni mzuri kwa sababu unarahisisha maelezo yake kama anavyosema. Hata hivyo, kuna utata katika uainishaji wa vijipera katika kila kipera. Kwa mfano, mivigha kama tunavyojua ni sherehe za kiibada au za kitamaduni zinazoambatana na matambiko fulani katika jamii teule. Yeye, ameweka kijipera hiki chini ya usimulizi. Aidha, mawaidha, vichekesho, sogu na malumbano ya utani yamepambanuliwa katika kipera cha tanzu fupi bila kueleza ufupi wake unaishia wapi.

Vilevile, King'ei na Kisovi (2005) wasema kuwa Fasihi Simulizi ya Waswahili imegawanyika katika tanzu tano: tanzu fupi, hadithi, hadithi fupi, maigizo na ushairi. Katika muainisho wao, wametenganisha hadithi fupi na hadithi kama tanzu zinazojitegemea na kutofautiana. Maelezo yao kuhusu hadithi fupi yanachanganya kidogo hasa wanapotoa mifano ya hadithi fupi kama vile khurafa, mazimwi na mbazi. Hii ni kwa sababu, mifano wanayotoa ni mirefu kulikoni ile wanayoitoa katika utanzu wa hadithi. Swali ni je, ufupi wa hadithi unakadiriwa vipi?

Kwa ujumla, wataalamu hawa wanakubaliana kuwa fasihi simulizi ya Waswahili ina tanzu kama vile nyimbo, mashairi, maghani, malumbano ya utani, methali, vitendawili, mivigha, tenzi na ngano na kadhalika. Uainishaji wao unatofautiana labda kwa sababu ya kutumia vigezo tofauti vya uainishaji. Hata hivyo, wote wanaibuka na idadi tofauti za tanzu na kuzitia tanzu zenyewe katika makundi tofauti tofauti. Kwa hivyo, tanzu hizi zinaingiliana sana hivi kwamba, ni vigumu kuziwekea mipaka dhahiri na ya kudumu. Hii ndio hali ya mwingilianotanzu ambayo imeshughulikiwa na Nadharia ya Tanzu. Aidha, wote wamekiri kuwa, uainishaji wao ni kwa ajili ya kutoa maelezo yenye mantiki tu. Chesaina (1997:11) anawaunga mkono kwa kusema:

Wambeere na Waembu waliainisha Fasihi Simulizi yao kwa mujibu wa utendakazi wake. Uainisho huo wa tanzu unaupa kila utanzu nguvu za kujitambulisha kutokana na silka zake za kipekee ili kurahisisha utafiti wa Fasihi Simulizi; kwani humsaidia mtafiti kuelekeza nguvu zake zote katika upekee wa utanzu husika.

Kadhalika, Mulokozi (1999:7) anasema:

Uainishaji wa tanzu si tatizo, ila tatizo lipo kwenye uainisho wa vipera chini ya kila utanzu, kwani ni vigumu kujua kipera kipi kinapaswa kuwekwa chini ya utanzu upi.

Naye, Miruka (2001:20), anapozungumzia ngano za Waluo anasema:

Nduni mojawapo ya ngano za Wajaluo ni uwepo wa nyimbo. Sio kwamba ngano zote huwa na nyimbo ila ngano nyingi huwa nazo.

Isitoshe, Finnegan (1970:76) anakiri hili kwa kusema:

Kuna tatizo la kutofautisha ngano na mashairi kwa sababu ngano zingine zinakaa kama mashairi nayo mashairi mengine yanakaa kama ngano. Jambo hili linanifanya nishindwe kuweka mipaka bayana kati ya tanzu hizi mbili. Hata hivyo, nimelazimisha uainisho huu ili niwe na muwala katika mawasilisho yangu. Aidha, lengo langu kuu sio kuainisha Fasihi Simulizi ya Kiafrika.

Msomi huyu maarufu ambaye ni mmoja kati ya watafiti waanzilishi wazuri wa Fasihi Simulizi ya Kiafrika anakiri kwamba amelazimisha utumikaji wa

muainisho wa kigeni kwa Fasihi Simulizi ya Kiafrika. Mjadala huu unaungwa mkono na Simiyu (2015:4) anaposema:

Ni vigumu kuweka mipaka bayana baina ya tanzu za fasihi simulizi; kwani kila utanzu huibuliwa, hukuzwa na kufifia ndani ya utanzu mwingine unaofanya vivyo hivyo ndani ya utanzu mwingine; katika mifanyiko hii ya mahusiano ya kingazi isiyokuwa na mwisho.

### Utata wa Kifasili

Utata mwingine unaotokana na uainishaji huu wa kigeni unahusiana na fasili mbalimbali za tanzu na vipera vya Fasihi Simulizi. Fasili za tanzu na vipera mbalimbali zilizotolewa na wataalam waliopitiwa katika utafiti huu ni za kimzunguko tu. Wataalam hawa wanaonekana kutaabika katika kujaribu kueleza maana ya tanzu kama vile methali, mivigha, vitendawili, nyimbo na maghani, bila mafanikio. Maelezo yao yanaongozwa na mawazo ya Aristole aliyejaribu kutoa fasili ya shairi, tamthilia na tanzia, (Wellek na Warren k.h.j). Yeye aliamini kuwa, tanzu hizi zilikuwa na sifa bainifu ambazo zingetumiwa kuzitofautisha. Kwa kuegemea mtazamo huu wa Aristotle, utanzu unaoitwa tarihi umefasiliwa na wataalam hawa hivi: Mulokozi (k.h.j) anasema kuwa, tarihi ni ngano zinazofafanua matukio ya kihistoria. Naye, Wamitila (k.h.j) anasema kuwa, tarihi ni hadithi ambazo husimulia au zimejengwa kwenye matukio ya kihistoria.

Fasili hizi zina maana kuwa, masimulizi yoyote kuhusu mambo yaliyotokea zamani ni tarihi. Hata hivyo, zipo tanzu zingine ambazo husimulia kuhusu matukio ya kihistoria. Kwa mfano, *Utenzi wa Al-Inkishafi* unasimulia kwa kina kuhusu matukio ya kihistoria yaliyojiri katika Ufalme wa Pate. Je, utenzi huu pia ni tarihi? Aidha, methali nyingi hufumbata masimulizi marefu ya matukio ya kihistoria katika ule ufupi wake. Je, ni kweli basi kusema kuwa, *methali ni tarihi iliyofufupishwa*? Kutokana na utafiti huu, inawezekana kabisa kuwa, methali zote zilibuniwa kutokana na ufupishaji wa tarihi au mighani.

Pili, baadhi ya fasili za wataalam mbalimbali kuhusu utanzu au kipera kimoja maalum zinakinzana, kama inavyodhihirika katika ufafanuzi wa dhana ya methali. Wamitila (k.h.j:135) anasema:

Methali ni msembo wa kimapokeo ambao una muundo fulani mahsusi, unaokumbukika na unaokusudia kueleza, kuadhibu, kusuta na kushauri.

Isitoshe, King'ei na Kisovi (k.h.j:29) wanasema:

Methali ni utungo wa kimafumbo unaofananisha dhana mbili. 'Methali' linatokana na kitenzi 'mithilisha', yaani fananisha au husisha.

Naye, Miruka (k.h.j:110) anadai:

Methali ni kauli fupi yenye maana fiche, inayokubalika na kutumiwa na jamii kama kiashiria cha ukweli na hekima.

Kadhalika, Chesaina (2003:17) anafafanua:

Methali inaweza kufasiliwa kama msemu mfupi wenye busara.

Hizi ni baadhi tu ya fasili za dhana ya methali. Wamitila anasisitiza ukale, uwezo wa kukumbukika kutokana na umbo maalum pamoja na majukumu yake, japo anataja machache tu. Ina maana methali ni tanzu za zamani tu na wala haziwezi kubuniwa kadiri muda unavyosonga mbele. Vilevile, mwandishi huyu hasemi huu ukale unaishia wapi. Halafu, anachanganya maana na dhima ya methali kana kwamba hizi zote ni sehemu za fasihi ya methali, wakati hivi ni vitu viwili tofauti. Kadhalika, King'ei na Kisovi wanashadidia umafumbo na ufananishaji bila kutaja muundo wala majukumu ya methali. Kulingana nao, kauli yoyote ambayo inatolewa kwa njia ya mafumbo na iwe inalinganisha dhana mbili ni methali. Pia, Miruka anataja mambo matatu muhimu kuhusu maana ya methali: ufupi, ufiche na maudhui ambayo lazima yawe ya kweli na yenye hekima. Hatimaye, Chesaina anasisitiza mambo mawili tu, ambayo ni ufupi na busara. Fasili hizi zikitazamwa kwa undani, ni kama zinafafanua vitu vinne tofauti wakati zinalenga kueleza maana ya dhana moja tu ya methali. Mfano wa pili unahusu fasili ya ushairi kwa mujibu wa wataalam hawa: Abedi (k.h.j:vii) anadhihirisha utata uliopo katika kufasili na kuainisha tanzu za fasihi kwa kudai:

Shairi au utenzi ni wimbo. Hivyo, kama shairi haliimbiki, halina maana. Kwani ingefaa asiyeweza kutunga mashairi sawasawa aeleze fikira zake kwa maelezo ya desturi kuliko kujitia ndani ya mkorogano wa maneno yasiyoimbika.

Abedi (k.h.j:12) anawakanganya wasomaji wake zaidi anapobadilika tena na kusema:

Neno utenzi maana yake ni ushairi wenye mizani michache kuliko kumi na mbili.

Kwa mujibu wa maelezo ya Abedi, hakuna tofauti kati ya utenzi, shairi na wimbo. Vilevile, mtaalam huyu hajasema istilahi hizi zinamaanisha nini, mbali na kutoa maelezo ya kimzunguko tu ambayo hayatoi fasili maalum. Na kama ni kweli kuwa hakuna tofauti kati ya tanzu hizi, kwa nini basi tuwe na majina matatu yanayosimamia kitu kilekile? Naye, Abdalla (1976:15) anashadidia mtafaruku huu wa kutotofautisha istilahi hizi kwa kusema:

Katika ushairi wa Kiswahili, idadi ya tungo za tenzi zilizo na maudhui ya kidini ni ndogo mno hata zahesabika.

Vilevile, Chiraghdin (1971:7) anawaunga mkono wenzake kwa kushindwa kusema kwa tafsili maana ya shairi anapodai:

Mashairi yana mshindo na mdundo yakiwa yanasemwa, yanaimbwa au yanasomwa. Basi yamkini sana kuwa, asili ya mashairi ya Kiswahili ni nyimbo.



Mjadala huu kuhusu maana ya shairi, unakolezwa zaidi na wanamapinduzi wanaoibuka na fasili tofauti ya shairi, kwa lengo la kujitofautisha na wanajadi. Kwa mfano, Mulokozi na Kahigi (1979:25) wanasema:

Ushairi ni sanaa inayopambanuliwa, kwa mpangilio maalum wa maneno fasaha na yenye muwala, kwa lugha ya mkato, picha au sitiari au ishara, katika usemi, maandishi, au mahadhi ya wimbo, ili kueleza tukio au hisi fulani, kuhusu maisha au mazingira ya binadamu, kwa njia inayogusa moyo.

Maelezo ya Mulokozi na Kahigi yanawaingiza kwenye mtego uleule wa kufasili shairi kwa misingi ya mtazamo wa Aristotle. Ila, wao pia wanaishia katika kutoa maelezo ya kimzunguko tu kuhusu maana ya shairi; hivi kwamba ni vigumu kusema kwa hakika maana ya shairi. Wanachanganya maana, sifa, namna ya uwasilishaji na wajibu wa shairi katika fasili yao; hivyo kushindwa kusema kwa tafsili shairi ni nini.

Zaidi ya huu mtafaruku wa kifasili, tanzu kama vile methali, visasili, tarihi na misemo zinaweza kuwakilishwa kwa neno moja tu katika utendaji. Tena, methali, misemo na misimu inaweza kuwasilishwa kupitia kwa maelezo marefu yenye mfumo wa kihadithi au yenye lugha ya kishairi. Hii ina maana, ni vigumu kusema kuwa utanzu fulani una muundo au umbo maalum lisilobadilika. Kwa hivyo basi, muundo na maana ya utanzu wowote ule wa Fasihi Simulizi hubadilika kulingana na matumizi yake katika muktadha wa utamaduni wa jamii maalum. Hakuna fasili moja sahihi ya utanzu wowote ule wa Fasihi Simulizi ya Kiafrika kwa sababu, maana na muundo wa kila utanzu hubadilikabadilika katika utendaji. Kimsingi, Fasihi Simulizi ni mfumo ambao umejengwa na tanzu ambazo zinaingiliana hivi kwamba haziwezi kutenganishwa; jambo ambalo linaweza kufafanuliwa vizuri na dhana ya mwingilianotanzu, kama nguzo mojawapo ya Nadharia ya Tanzu.

#### **Utata wa Kitaaluma**

Kuna baadhi ya “tanzu” zilizoshughulikiwa na wataalam hawa ambazo zikichunguzwa kwa makini, ni ama majukumu ya Fasihi Simulizi; vipengele vya fani vinavyotumiwa kuwasilisha Fasihi Simulizi; majukwaa yanayoruhusu utendaji wa Fasihi Simulizi; au aina ya sanaa tofauti kabisa na Fasihi Simulizi. Tumejadali masuala haya kama ifuatavyo:

#### **Majukumu ya Fasihi Simulizi au Tanzu za Fasihi Simulizi?**

Wataalam tuliwarejelea wameyageuza baadhi ya madhumuni ya Fasihi Simulizi na kuyajadili kama tanzu za Fasihi Simulizi kimakosa. Baadhi ya “tanzu” hizi ni kama vile mawaidha. Wamitila (k.h.j) anadai kuwa, mawaidha ni maneno ya maonyo au mafunzo aghalabu huwa ya kidini na yenye mwongozo. Manaeno haya hutumika kuonya au kutoa mwongozo. Naye Simiyu (k.h.j) anasema kwamba, mawaidha ni mashauri ya kunasih, kuasa, kuonya au kuelekeza na

hutolewa mbele ya hadhira kupitia mbinu ya masimulizi pamoja na tanzu nyingine za Fasihi Simulizi kama methali, nyimbo, mafumbo, ngano, vitendawili au vichekesho. Kipera hiki kimiwekwa chini ya utanzu wa maigizo na wataalam kama vile Mulokozi (k.h.j), Wamitila (k.h.j) na Simiyu (k.h.j).

Kutokana na maelezo ya hawa wataalamu kuhusu maana ya mawaidha, imebainika kuwa, mawaidha huwasilishwa kupitia kwa tanzu au vipera kama vile methali, nyimbo, ngano na vitendawili. Hii ina maana tanzu za Fasihi Simulizi zinaweza kutumiwa kutoa mawaidha. Kwa mfano, methali kama, '*Akunyimaye mbaazi kakuepushia mashuzi*' inaweza kutumiwa kuwapa watu ambao walikosa kupata kitu fulani maishani, kwamba wasitie shaka maana wangepata kitu chenyewe wangepata shida. Vilevile, nyimbo za harusi zinaweza kutoa mawaidha kuhusu unyumba; nyiso zikatoa mawaidha kuhusu utu uzima; na hekeya zikatoa mawaidha kuhusu tahadhari maishani. Haya yanabainika katika Simiyu (k.h.j:23) anaposema:

Fasihi Simulizi hutekeleza majukumu mbalimbali yakiwemo: Kueneza na kuhifadhi mila, desturi na amali za jamii, kuburudisha na kutumbuiza jamii, kuendeleza na kukuza lugha, kutoa maadili, **mawaidha** na mafunzo mbalimbali kwa kuonya, kusifu au kukashifu mambo fulani katika jamii, kueneza ushirikiano na utangamano katika jamii pamoja na kutambulisha jamii husika.

Kwa hivyo basi, mawaidha sio utanzu wala kipera cha Fasihi Simulizi bali ni majo kati ya majukumu yanayotekelezwa na Fasihi Simulizi katika jamii. Mawaidha haya yanaweza kutolewa kama sehemu ya maudhui ya tanzu mbalimbali za Fasihi Simulizi.

### Vipengele vya Fani au Tanzu za Fasihi Simulizi?

Baadhi ya kazi tulizorejelea zinapambanua vipengele vya fani kama vile mafumbo kama tanzu au vipera vya Fasihi Simulizi. Mafumbo kama kipera cha fasihi simulizi kimefanunuliwa hivi: Simiyu (k.h.j) anasema kuwa, mafumbo ni semi ambazo maana yazo imefichika kabisa na huhitaji umakini na maarifa kuifumbua. Fumbo huhitaji jibu papo kwa hapo. Kuna mafumbo ya kimapokeo na ya kisasa. Hata hivyo, King'ei na Kisovi (k.h.j:29) wanasema:

Methali ni utungo wa **kimafumbo** unaofananisha dhana mbili. 'Methali' linatokana na kitenzi 'mithilisha', yaani fananisha au husisha.

Aidha, Mulokozi (k.h.j:30) anadai:

Istiara ni hadithi ambayo maana yake ni wazi inawakilisha maana nyingine iliyofichika kwani hutumia lugha ya **kimafumbo**.

Kadhali, utafiti huu umethibitishwa kuwa, dhana hii ya 'utanzu' haina mashiko dhahiri katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika katika hali halisi ya utendaji. Hili linaungwa mkono na McCaskie (1989) anapofanua maana ya *asantesem*

kwa kusema kuwa, *asantesem* ni neno, maongezi, hotuba, msemo, ngano, hadithi, historia, utamadumi, maudhui n.k. Naye Bulman (1989:171) anashadidia ukweli wa kualii hii kwa kusema:

Afadhali nitumie istilahi ‘kisa’ kwa maana ya *The Buffalo-Woman Tale* badala ya istilahi kama vile mighani, kisasili, khurafa au ngano, kwa sababu, istilahi hizi hujikita katika maana majowapo tu ya utanzu huu.

Hii ina maana kwamba, tanzu zote za fasihi huwa na umafumbo fulani ambao unazifanya ziwewe chini ya sanaa ya fasihi. Tanzu kama vile methali, misemo, ngano na nyimbo hujengwa katika fumbo fulani kuhusu maisha.

### **Taaluma Nyinginezo au Tanzu za Fasihi Simulizi?**

Marejeleo yetu yanaonesha kuwa, kuna baadhi ya wataalam waliobainisha ‘tanzu’ ambazo sio sehemu ya taaluma ya Fasihi Simulizi bali ni aina tofauti kabisa ya sanaa. Ni kweli kwamba Fasihi Simulizi ni aina ya sanaa, ila sio sanaa zote zinazoweza kuitwa Fasihi Simulizi. Kwa mfano, Baba wa uainishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiswahili, Kirumbi (k.h.j) amegawa Fasihi Simulizi ya Kiswahili katika fani kumi na mbili: hadithi, tamthilia, ushairi, nyimbo, mithali/semi/misemo, utani, unyago, michezo, posa na ndoa, uchawi na uganga, vitendawili na utabibu. Muainisho wake ni mzuri kwa sababu ni mpana ila unakanganya kwelikweli. Kwanza kabisa, kuna vipera ambavyo vinastahili kuwekwa katika utanzu mmoja kama vile nyimbo na ushairi; na vitendawili, mithali na misemo. Aidha, kuna fani ambazo tunafikiria si sehemu ya Fasihi Simulizi. Kwa mfano, michezo ambayo anasema inajumuisha miereka, kivumbizi, kufuma kwa mishale na kuogelea pwani. Kwa maoni yetu, hii si sehemu ya fasihi wala Fasihi Simulizi lakini ni sehemu ya sanaa. Aidha, uchawi, uganga, posa na ndoa si sehemu ya Fasihi Simulizi ijapo shughuli hizi huendeshwa kwa kutumia tanzu mbalimbali za Fasihi Simulizi kama vile nyimbo na methali. Vilevile, tamthiliya ni utanzu wa fasihi andishi.

### **Majukwaa au Tanzu za Fasihi Simulizi?**

Majukwaa ni miktadha maalum inayoelekeza uteuzi na uwasilishaji wa tanzu za Fasihi Simulizi ili ziweze kutekeleza wajibu wake vyema. Majukwaa haya ni pamoja na jukwaa la kuzaliwa, jukwaa la ujinaishaji, jukwaa la kivuko, jukwaa la ndoa na jukwaa la kifo. Majukwaa haya yanaweza kuruhusu utendaji halisi au uigaji wa utendaji wa tanzu za Fasihi Simulizi. Kutegemea na jukwaa maalum, utanzu au tanzu za Fasihi Simulizi zinawaze kuwasilishwa kama maigizo, michezo jukwaani mazungumzo au mivigha. Tunajadili kila kipengele kama ifuatavyo:

### **Maigizo**

Simiyu (k.h.j) anasema kuwa maigizo ni masimulizi yanayoambatana na matendo kwenye jukwaa mbele ya hadhira. Kama ilivyo katika maisha yetu ya kawaida,

watu huigiza jinsi watu wengine wanavyofanya mambo; kama vile mtoto kujifunza kufanya mambo kwa kuiga wazazi. Kadhalika, Mulokozi (k.h.j) anadai kwamba, maigizo ni michezo ambayo hutumia watendaji wa kuiga tabia na matendo ya watu au viumbe wengine ili kuburudisha na kutoa ujumbe fulani kwa hadhira. Maigizo hutumika kuburudisha, kuelimisha au kuonya. Mandhari huambatana na matukio maalumu kama vile kwenye maadhimisho ya sherehe fulani na katika matukio ya kijamii. Maigizo hufanywa kwa madhumuni ya kuwasilisha ujumbe fulani katika jamii kwa njia ya matendo.

Kwa hivyo, utafiti huu unaonyesha kuwa, ‘utanzu’ uitwao ‘maigizo’ sio ‘utanzu’ unaoweza kujisimamia bali ni jukwaa ambalo hutumiwa na tanzu zingine wakati wa utendaji. Hii ndio maana, ninatilia shaka uainishaji wa Ki-Aristotle, ambao umetumiwa na watalaam mbalimbali katika kuweka mipaka bayana katika ya tanzu za Fasihi Simulizi ya Kiafrika, wanaoutambua ‘utanzu’ wa ‘maigizo’. Kutokana na maelezo haya, maigizo ni uigizaji wa mambo mbalimbali katika jamii, zikiwemo tanzu za Fasihi Simulizi. Kwa mfano, fanani chipukizi anaweza akiuga sauti na minenguo ya Mama wa Taarab Saida Karoli. Ikitokea hivyo basi, maigizo ni jukwaa linaloruhusu uteuzi na utolewaji wa nyimbo wakati wa utendaji wake.

### **Mazungumzo**

Mulokozi (k.h.j) anasema kuwa, mazungumzo ni maongezi au maelezo ya mdomo katika lugha ya kawaida juu ya jambo lolote lile. Lugha iliyotumika ni ya kifasihi. Muundo wake huwa wa kidayalojia. Ni maongezi kati ya mtu mmoja na mwingine au watu wengi, ambayo ndio njia kuu ya maingiliano baina ya binadamu. Mazungumzo huwa na lengo maalum ambalo ni kuwasiliana.

Kulingana na Mulokozi basi, sio fasihi ila mzungumzaji akiwa hodari anaweza kuingiza vipengele vya fasihi simulizi kama vile methali na misemo. Hivyo basi, mazungumzo ni jukwaa linalotoa fursa ya kuruhusu utolewaji na uwasilishaji wa fasihi simulizi katika utendaji.

### **Mivigha**

Mivigha ni kati ya tanzu tatanishi. Wamitila (k.h.j) anafasili mivigha kama sherehe zinazofanywa katika jamii yoyote teule na hufungamana na tamaduni za jamii husika pamoja na matambiko ya aina yake. Ukweli huu unafafanuliwa vizuri na Kirumbi (1975:39) anaposema:

Unyago ni fani nyingine ya aina ya pekee katika jamii yetu. Jamii yetu iliona umuhimu wa fani hii ambayo imekuwepo siku nyingi sana kabla ya hao wanaoitwa “walioendelea na waliostaarabika” kuona umuhimu wa *sex education* iliyopotoshwa.

Mivigha hujengwa kwa fito za malumbano ya utani, nyimbo, majigambo, mighani na maghani yanayoshirikiana na kuingiliana kuanzia mwanzo hadi

mwisho. Kwa hakika, haiwi mivigha iwapo tanzu hizi zitaondolewa. Ikitokea hivyo, basi mivigha husika itasalia kuwa kuvu ambalo halina muundo wala maudhui yoyote. Ni huu mwingiliano wa tanzu ndogondogo ndani ya tanzu kubwa kiasi ndio unaojenga na kuamilisha mivigha. Barber (1989:18) anaunga hili mkono kwa kusema kuwa, *oriki* haina mwisho wala mipaka dhahiri kwani, *oriki* ni kama mkoba mkubwa unoweza kumeza tanzu zingine kama vile methali, mashiri na vitendawili... tanzu hizi ndani ya *oriki* hazina uhusiano wa moja kwa moja, ila zinaletwa pamoja kutokana na maudhui lengwa. Kwa hivyo, utanzu unaoitwa ‘mivigha’ haupo; badala yake ‘utanzu’ huu unafaa kuangaliwa kama jukwaa linaloruhusu utolewaji wa tanzu mbalimbali zinazoingiliana katika utendaji. Hii ni kwa sababu, ‘utanzu’ wa mivigha ni kama basi linalobeba abiria kuelekea sehemu mbalimbali. Kila abiria hupanda basi hili katika vituo tofautitafauti na anapofika anakoenda, abiria huyo hushuka huku akiwaacha wasafiri wengine wakiendelea na safari. Hii ina maana kuwa, ‘mivigha’ sio utanzu bali ni kongoo la Fasihi Simulizi linaloelea na ambalo ‘tanzu’ mbalimbali hupanda jukwaani na kutekeleza wajibu wake, na baadaye kushuka au kushushwa ili kupisha tanzu zingine; nazo zitekeleze wajibu wake. Upandaji na ushukaji huu wa tanzu hizi huiwezesha ‘mivigha’ ya *embalu* na *mwaka kogwa* kutekeleza wajibu wake wa kiujumla.

Ni wazi kwamba, kuna utata katika kufasili na kuainisha Fasihi Simulizi ya Kiafrika kwa mujibu wa wataalam mbalimbali niliowapitia. Utata huu pia unadhihirika katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi katika taasisi mbalimbali za elimu. Hili ni tatizo linalotokana na athari ya muainisho wa kigeni ambao haulandani na kazi za Fasihi Simulizi ya Waafrika. Tatizo hili linatokana na hali ya Waafrika wanaopenda sana kuyaangalia na kuyaona mambo yao kwa kutumia miwani ya kuazima ili waonekane kuwa wanakwenda na wakati, badala ya kutumia mitazamo yao faafu. Okpewho (1992) analikubali wazo hili na kupendekeza kuwa, mfumo wa uainishaji na uchanganuzi wa Fasihi Simulizi unapaswa kutambulika na kukubalika na jamii husika. Si hivyo tu, ninapendekeza kuwa, utafiti na uchanganuzi mwafaka wa Fasihi Simulizi unafaa kufanywa kwa kuegemea maarifa na tajiriba ya wazawa wa jamii tafitiwa. Hii ni kwa sababu, kutokana na tajiriba na muktadha wao wa malezi, wazawa wana nafasi nzuri zaidi ya kujaliza mapengo na ukimya unaopatikana katika fasihi husika; kama wanavyopendekeza waitifaki wa Nadharia ya Muono-Ndani.

### **Mustakabali wa Kisasa wa Uainishaji na Fasihi Simulizi**

Wataalam wengi wa kigeni na wenyeji bado wanatumia nadharia na mbinu za Kiaristotle katika uainisho wao wa Fasihi Simulizi ya Kiafrika. Wataalam hawa ni pamoja na Finnegan (2012), Ong’ (1982), Bayo na Abadul Rashid (2012), Liz na Graham (1995), Namulundah (2012) na wengine. Inaonekana hakuna juhudi zozote za kuboresha mtazamo huu wa uainisho wa Fasihi Simulizi ya Kiafrika. Okpewho (1992) analikubali hili kwa kusema:

Mfumo wa uainishaji wa Fasihi Simulizi unapaswa kutambulika na kukubalika na jamii husika. Tunapaswa kutumia sifa na mila zinazozifananisha jamii mbalimbali katika kuainisha Fasihi Simulizi.

Sisi hatulengi kupinga tu na kutupilia mbali muainisho ambao upo, bali tunanua kuuboresha. Tunaamini kwamba, katika hali halisi ya utendaji wa Fasihi Simulizi, muainisho huu hauna nafasi na kwa hivyo kuna haja ya kufikiria upya juu ya uainishaji wa Fasihi Simulizi. Tunapendekeza kuwa uainishaji wa Fasihi Simulizi ufanywe kwa kuiangalia Fasihi Simulizi kama mfumo kamili wa maarifa. Mfumo huu unajengwa na tanzu na vipera ambavyo vinaingiliana, kutagusana, kutengua na kutegemeana sana na haviwezi kutenganishwa. Uainisho huu unapaswa kuambatanishwa na matambiko ya kitamduni: kuzaliwa, kuwapa watoto majina, kubalehe, tohara/ukeketaji/kung'oa meno, kuchumbiana na kuoa, kusimika watemi, kuadhimisha ufanisi, maziko na kumbumbuku. Matambiko haya hurusu mwingiliano wa tanzu na vipera maalum. Hili linaungwa mkono na Senkoro (2011) anaposema:

Inawezekana kabisa kuwa tanzu za Fasihi Simulizi ya Kiafrika hazipaswi kuainishwa moja moja. Kutumiwa kwa utanzu mmoja wa Fasihi Simulizi katika utolewaji wa utanzu mwingine ni mbinu ya kifani itumiwayo na wasanii wa fasihi.

Mifano hii inadhihirisha wazi kuwa fasihi simulizi ni mfumo madhubuti wa elimu usioweza kutenganishwa katika vijischemu vinavyojisimamia. Huenda mbinu za kitaaluma ambazo tumezoea kuzitumia katika kuainisha vitu kwa kuviwekea mipaka bayana hazina nafasi katika uainishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiafrika katika hali halisi ya utendaji. Sisi tunapendekeza kwamba, wataalam wasijisumbue na uainishaji wa Fasihi Simulizi katika tanzu moja moja kwani hawatafuadafu; badala yake wajishughulishe zaidi na utendakazi wake kama mfumo kamilifu wa elimu ndani ya tambiko maalum linalotambulika na jamii maalum. Inaonekana tanzu na vipera vya Fasihi Simulizi vinafanya kazi kama mfumo mmoja mkubwa ambao vijischemu vyake haviwezi kutenganishwa! Aidha, huenda mbinu za kitaaluma ambazo tumezoea kuzitumiwa katika kufasili, kuainisha na kuchunguza vitu kwa kuviwekea mipaka bayana, hazina nafasi katika fasili, uainishaji na uchambuzi wa Fasihi Simulizi ya Kiafrika katika hali halisi ya utendaji.

Inasadikiwa kuwa, wataalam hawapaswi kujisumbua kwa kutaka kufasili, kuainisha na kuchambua Fasihi Simulizi ya Kiafrika katika tanzu moja moja kwani hawatafuadafu; badala yake wajishughulishe zaidi na utendakazi wa Fasihi Simulizi ya Kiafrika kama mfumo timilifu wa elimu ndani ya 'mivigha' maalum inayotambulika na jamii maalum. Imedhihirishwa kwamba, tanzu na vipera vya Fasihi Simulizi vinafanya kazi kama mfumo mmoja mkubwa ambao vijischemu

vyake haviwezi kutenganishwa asilani! Suala hili linapaswa kutiliwa maanani katika ufundishaji wa Fasihi Simulizi katika viwango mbalimbali vya elimu.

### Hitimisho

Kutokana na mjadala unaoendelezwa ninapendekeza kuwa, uainishaji na uchambuzi wa Fasihi Simulizi ya Kiafrika unapaswa kufanywa kwa kuchukulia Fasihi Simulizi ya Kiafrika kama mfumo timilifu wa maarifa unaoundwa kwa ‘tanzu’ dhahania. Mfumo huu hujengwa kwa ‘tanzu’ na ‘vipera’ ambavyo huingiliana, kujinyambua, kutenguana na kuingiliana kikorasi na kimatini, hivyo, haviwezi kutenganishwa katika utendaji. Aidha, uainishaji na uchambuzi huu unapaswa kuongozwa na ukweli kuwa, ‘mivigha’ mbalimbali ndio hutumiwa kama jukwaa la utendaji: kuzaliwa, kuwapa watoto majina, kubalehe, tohara au ukeketaji au kung’oa meno, kuchumbiana na kuoa, kusimika watemi, kuadhimisha ufanisi, maziko pamoja na kumbumbuku. Matambiko haya huruhusu udhihirikaji wa mwingiliano wa ‘tanzu’ na ‘vipera’ maalum katika utendaji.

Inaonekana hakuna juhudi za kimakusudi za kuboresha mtazamo huu wa uainishaji wa Fasihi Simulizi ya Kiafrika. Tunapaswa kutumia sifa na mila zinazozifananisha na kuzitofautisha jamii mbalimbali katika kuainisha Fasihi Simulizi yao. Silengi kupinga tu na kutupilia mbali muainisho ambao upo, bali ninanua kuuboresha. Ninaamini kwamba, katika hali halisi ya utendaji wa Fasihi Simulizi ya Kiafrika, muainisho huu hauna nafasi na kwa hivyo, kuna haja ya kufikiria upya.

### Marejeleo

- Abedi, K. A. (1954). *Sheria za Kutunga Mashairi na Diwani ya Amri*. Nairobi: E. A. L. B.
- Barber, K. (1989). Interpreting *Oriki* as History and as Literature katika Barber, K. na Farias, P. F. (1989). (Wah). *Discourse and its Disguises: The Interpretation of African Oral Text*. Birmingham: Centre of West African Studies.
- Bulman, S. (1989). *The Buffalo-Woman Tale: Political Imperatives and Narrative Constraints in the Sunjata Epic*, katika Barber, K. na Farias, P. F. (1989). (Wah). *Discourse and its Disguises: The Interpretation of African Oral Text*. Birmingham: Centre of West African Studies.
- Chesaina, C. (1997). *Oral Literature of The Embu and Mbeere*. Nairobi: E. A. E. P. Ltd.
- Finnegan, R. (1970). *Oral Literature in Africa*. Nairobi: Oxford University Press.
- Kimani, W. na Chimera R. (1999). *Ufundishaji wa Fasihi; Nadharia na Mbinu*. Nairobi: Jomo Kenyatta Foundation.
- King’ei, G. K. na Kisovi C. (2005). *Msingi wa Fasihi Simulizi*. Nairobi: K. L. B.
- Kirumbi, P. (1975). *Misingi ya Fasihi Simulizi*. Nairobi: Shungwaya Publishers Ltd.

- Liz, G. na Graham F. (1995). *Power, Marginality and African Oral Literature*. Chuo Kikuu cha London.
- Madumulla, S. J. (1995). *Proverbs and Sayings; Theory and Practice*. Dar es Salaam: Institute of Kiswahili Research.
- McCaskie, T. C. (1989). "Asantesem": *Reflections on Discourse and Text in Africa*, katika Barber, K. na Farias, P. F. (1989) (Wah). *Discourse and its Disguises: The Interpretation of African Oral text*. Birmingham: Centre of West African Studies.
- Miruka, O. (2001). *Oral Literature of The Luo*. Nairobi: E. A. E. P. Ltd.
- Muller, W. G. (1991). *Interfigurity: A Study on the Interdependence of Literary Figures*, katika Plett, H. F. (1991). (Mh). *Intertextuality*. Berlin: Walter de Gruyter.
- Mulokozi, M. M. (1996). *Utangulizi wa Fasihi*. Dar es Salaam: TUKI.
- Mulokozi, M. M na Kahigi, K. K. (1979). *Kunga za Ushairi na Diwani Yetu*. Dar es salaam: TPH.
- Namulundah, F. L. (2011). *The Bukusu of Kenya: Folktales, Culture and Social Identities*. Carolina: Carolina Academic Press.
- Ngure, A. (2003). *Fasihi Simulizi kwa Shule za Sekondari*. Nairobi: Phoenix Publishers.
- Okpewho, I. (1992). *African Oral Literature: Background, Character and Continuity*. Indiana.
- Ong, W. J. (1982). *Orality and Literacy*. Chicago: Methuen and Company Ltd.
- Senkoro, F. E. M. K. (2011). *Fasihi*. Dar es Salaam: KAUTTU Ltd.
- Simiyu, F. W. (2011). *Kitovu cha Fasihi Simulizi: Kwa Shule, Vyuvo na Ndaki*. Mwanza: Serengeti Educational Publishers (T) Ltd.
- Simiyu, F. W. (2015). Mwingilianotanzu katika Fasihi Simulizi ya Kiafrika: mfano wa *Embalu na Mwaka Kogwa*. Tasnifu ya Uzamifu: Ndaki ya Kenyatta.
- Wamitila, K. (2003). *Kichocheo cha Fasihi*. Nairobi: Phoenix Publishers Ltd.